# STANDARD 7 MID TERM 2 EXAM 2019

# KISWAHILI

Toleo la 0052019 DARASA LA SABA KISWAHILI Muda :1saa 40 dakika

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nambari 1hadi 15 zilizoachwa wazi. Kwa kila nafasi jaza kwa jibu sahihi.***

Mzee Jitumbo ndiye ajuaye _____1_____ ukweli wa methali _____2_____. Jitumbo _____3_____ pesa, akawa maarufu kote kitongojini. Alijaliwa kupata mali _____4_____ ajabu. Alikuwa na maduka kadhaa ya kuuzia _____5_____ za kilimo na mitambo ya kusaga mahindi. _____6_____ kilimfunika polepole na kuwaona wengine _____7_____ wasio na akili. Hatimaye ilibainika kuwa alikuwa _____8_____ mkubwa aliyeiba mali ya umma. Mali yote yakatwaliwa na kuachwa hoi!

1. A. kweli B. fika C. wasi D. pika
2. A. mpanda ngazi hushuka. B. akili ni mali. C. haba na haba hujaza kibaba. D. akiba haiozi.
3. A. alinukia B. alichelea C. aliengaenga D. alinuka
4. A. mingi B. anuwai C. mengi D. haba
5. A. sana B. zana C. vipuli D. vupuri
6. A. Kiburi B. Maringo C. Kinyongo D. Kiwewe
7. A. majabali B. mabingwa C. mazuzu D. jeta
8. A. padri B. msaliti C. mhuni D. fisadi

Ajira ya watoto _____9_____ vibaya kwa namna fulani kama vile kiakili, _____10_____ na kimakazi, _____11_____ kusahau maadili. Madhila _____12_____ watoto katika ulimwengu wa ajira za watoto duniani _____13_____. Hapa Afrika, karibu watoto milioni sabini na nane au _____14_____ ishirini na moja ya watoto wanahusika katika ajira _____15_____.

9. A. huwaathiri B. huwadunisha C. huwaadhiri D. huwasaidia
10. A. kimawazo B. kimwili C. kitabia D. kimavazi
11. A. lakini ni B. licha ya C. bighairi ya D. mathalani
12. A. inayowakumba B. itakayowakumba C. zinazowakumba D. yanayowakumba
13. A. ni chache B. si haba C. ni haba D. ni adimu
14. A. akisami B. asilia C. asilimia D. asili
15. A. kocho B. kibao C. kiduchu D. anuwai

***Kutoka swali la 16 hadi 30 , jibu swali kulingana na maagizo***

16. Tambua kundi lenye irabu **pekee**.
    A. ch, d, dh B. o, i, e
    C. ng, ny, th D. a, u, b

17. Ni nomino gani ambayo ni ya kufikiriwa tu?
    A. Mtoto B. Sukari
    C. Ualimu D. Damu

18. Ufuatao ni ukanusho wa **Hatukusoma kwa kuwa hatukufahamu**:
    A. Tulisoma kwa kuwa hatukufahamu.
    B. Hatukusoma kwa kuwa tulifahamu.
    C. Kusoma kwetu hakukuwezekana.
    D. Tulisoma kwa kuwa tulifahamu.

19. Katika neno **wanaorandaranda**, kirejeshi ni
    A. o B. wa
    C. na D. nda

KISW DARASA LA SABA 005 2019

20. Tambua jozi **isiyofaa**
A. Kijakazi - kitwana
B. Jogoo - koo
C. Ajuza - bikizee
D. Malkia - mfalme

21. Kamilisha methali ifuatayo:
**Kwendako mema**
A. hakina merejeo
B. ndio hatima ya yote
C. na mabaya hayakosi
D. hurudi mema

22. Chagua sentensi yenye kivumishi.
A. Alitembea chapuchapu hadi dukani.
B. Miti gani itakatwa kesho?
C. Waliocheka darasani ni watukutu.
D. Jitahidi ufike mapema.

23. Anayefanya kazi ya kutengeneza bidhaa zake kwa udongo ni
A. hatibu. B. mkutubi.
C. mfinyanzi. D. nokoa.

24. Ni nini maana ya sentensi ifuatayo:
**Dalali ameninadia bidhaa mnadani.**
A. Shughuli ilifanyiwa mahali fulani.
B. Shughuli ilifanywa kwa niaba yangu.
C. Shughuli ilifanywa kwa sababu yangu.
D. Shughuli ilikuwa yangu.

25. **Mwalimu: Masalkheri wanafunzi**
**Wanafunzi: Akheri mwalimu**
Bila shaka mazungumzo haya yalifanyika majira ya
A. asubuhi B. adhuhuri
C. jioni D. usiku


26. Tambua maelezo yaliyo sahihi
A. Chaka ni hali ya kitu kuwa kikuukuu.
B. Shaka ni msitu mkubwa.
C. Chaka ni hali ya kuwa na uhakika.
D. Shaka ni hali ya wasiwasi.

27. Chagua jina **lisilostahili** hapa.
A. Kitwitwi B. Keremkerem
C. Bukini D. Ninga

28. Tambua sentensi yenye kiwakilishi cha nafsi ya pili.
A. Nilikuona ulipoingia sebuleni
B. Mliochelewa mtaadhibiwa.
C. Yeye alicheza vizuri sana.
D. Wao hawakupenda masomo.

29. **"Visipoanguka havitaonekana"** Sentensi hii ipo katika hali ya
A. masharti
B. mazoea
C. amri
D. kutendatenda

30. Tambua maumbo haya.



A. Tao, kitovu, mche
B. Mche, tao, kitovu
C. Nusu mduara, kipenyo, mche
D. Mche, mduara, kitovu

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31hadi 40</u>***

Paukwa !.... Hapo zamani za kale kabla ya mawe kukauka, paliondokea jongoo na chura. Usuhuba wao ulikuwa shakiki! **<u>Waliandamana kama mtu na kivuli chake.</u>** Kulikuwa na jambo moja lililomsumbua chura moyoni. Kila alipotaka kumwuliza sahibu yake alishindwa ; aliogopa.

Siku moja, aliamua kulivua joho la woga na kuchukua hatua ya kishujaa. Akaanza , " Ndugu yangu , ngozi yako inapendeza sana. Inametameta metumetu kama kwamba umejipaka mafuta. Je. umetumia nini hadi ikawa hivyo?" Jongoo akamjibu , "Kwani unataka yako imetemete kama yangu?" "Ndio" chura akajibu. "Haya tega masikio nikueleze siri hiyo. Mimi huwasha moto kisha..." Chura akamkatizia , "Kisha unajirusha kwenye moto huo?"

"La sivyo, ngoja nimalizie" Jongoo akamsihi rafiki yake. "Haya endelea , nasikiliza," Chura akaomba ".... kisha huteleka chungu chenye mafuta ya nazi, yakishachemka mimi hu..."chura akamkatizia tena , "Hujirusha ndani haraka bila kupoteza wakati?" "Ndio . Hivyo ndivyo mie hufanya!" Jongoo akajibu kwa hasira.

Jibu hilo lilimpa chura furaha ghaya. Akachana mbuga hadi kiamboni. Mara moja akawasha moto, akatia mafuta ya nazi chunguni yakachemka chemchem! Bila kubananga muda, huyoo! Akajitumbukiza ndani! Kwani ilimchukua muda humo ndani? Aliruka nje ya chungu akiwa amechomeka mwili mzima. Ilimchukua mwaka kupona majeraha hayo. Maskini chura, ngozi yake ikawa na mabaka mabaka. Ikawa mbaya kuliko ilivyokuwa hapo mbeleni kabla ya mkasa huo.

Compiled & supplied by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com

Jongoo alikuwa na uhakika mambo hayakuwa shwari kwa kutomwona mwandani wake kwa muda mrefu. Hivyo akaamua kumtembelea chura ili kumpiga jicho mwandani wake aliyempotelea. Chura akaanza kulalamika, " Kumbe wewe ni adui yangu!, Unataka nijiue? Mbona ukanipa mbinu ambayo imeharibu ngozi yangu badala ya kuifanya imetemete na kuvutia?"

"Mimi nilitaka kukueleza vile nifanyavyo lakini ukakosa subira. Unarukia maneno na kutoa majibu hata kabla sijamaliza. Sasa nisikilize ambavyo mie hufanya." Akamweleza kwa makini. Chura hakumkatiza; ukweli ukawa...

31. Kulingana na aya ya kwanza, huenda chura alishindwa kumwuliza jongoo swali kutokana na
A. udogo wa jongoo
B. heshima aliyompa jongoo
C. woga kwa jongoo
D. shaka la urafiki wao

32. Kauli **<u>" Waliandamana kama mtu na kivuli chake"</u>** inaashiria
A. walishirikiana katika mambo yote.
B. walifanya kazi pamoja.
C. hakuna lililowatenganisha.
D. walipendana sana.

33. Ngozi ya jongoo iliyompendeza chura ilitokana na
A. mafuta aliyojipaka.
B. kujirusha katika moto.
C. usafi wake wa mwili.
D. umbo la ngozi yake.

34. Chura alikuwa na hulka ya kuuingilia au kuukatiza usemi na jongoo, hivyo ni sahihi kusema
A . chura alimkata kauli jongoo.
B. jongoo alimkata kauli chura.
C. chura alikata shauri.
D. jongoo alimkata chura maneno.

35. Maelezo ya jongoo kwa chura
A. yalikuwa nusu.
B. yalikuwa yamefika mwisho.
C. yalitosheleza.
D. yalikamilika.

36. Kilichomfurahisha chura mwishowe
A. kilimfaa zaidi.
B. kilimhuzunisha jongoo.
C. kilimfaa jongoo.
D. kilimletea majuto.

37. Tabia ya chura ilijawa na
A. umakinifu.
B. majuto.
C. pupa.
D. majonzi.

38. Chura alishindwa kustahimili joto la mafuta yale ndiposa
A. akalalamika.
B. akaruka nje ya chungu.
C. ngozi yake ikaharibika.
D. akamlaumu Jongoo.

39. Kutokana na kisa ulichokisoma, chura
A . alipenda sana ngozi yake ya asili.
B. jongoo hakuipenda ngozi yake ya asili.
C. chura hakuipenda sura yake ya asili.
D. chura hakuipenda ngozi ya jongoo ya asili.

40. Methali inayoweza kutumika kukamilisha kifungu hiki ni
A. Mwiba wa kujidunga hauna pole.
B. Haba na haba hujaza kibaba.
C. Maji yakimwagika hayazoleki.
D. Akikalia kigoda mtii.

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 hadi 50***

Tarakilishi ina sifa nyingi muhimu ambazo **tutaziweka bayana**. Chombo hiki kina uwezo wa kufanya hesabu na kazi nyingine nyingi kwa kasi sana. Aidha, tarakilishi huhifadhi ujumbe mwingi sana kwa matumizi ya baadaye.Maelekezo huchukuliwa na kuwekwa kwa ajili ya kufuatwa na chombo hiki. Mfululizo wa maelekezo haya ndio huongoza kompyuta katika kutekeleza wajibu wake na huitwa programu ambayo huandikwa kwa lugha ya kikompyuta. Kompyuta hufuata maelekezo haya kwa kuamrishwa na binadamu. Sheria hizi huwa sahili yaani zisizo ngumu, na kompyuta ina uwezo wa kuzitumia ili kufikia uamuzi wa jinsi ya kutenda.

Kuwasiliana na mifumo mingine ya kompyuta ni muhimu sana na kompyuta ina uwezo wa kufanya hivyo, jinsi wafanyavyo wanadamu. Kompyuta huingizwa taarifa zinazoonyesha hali halisi zikiwa katika maelezo au takwimu na hatimaye huchakatwa ili kutoa maana. Zao la programu huiwezesha kompyuta kuchukua data na kuifanya iwe habari.

Katika kompyuta, habari inaweza kuhifadhiwa katika diski ngumu au diski tepetevu. Diski ngumu ni inayopatikana katika kompyuta yenyewe na ina uwezo wa kuhifadhi maktaba nzima. Diski tepetevu ni ile nafasi ambamo disketi huwekwa ili habari inayochakatwa ihifadhiwe kwa disketi.

---

**41.** Kulingana na kifungu ni sifa gani ambayo mwandishi **hajaipa** kompyuta?
- A. Shughuli zake hafanyika upesi.
- B. Kuweka ujumbe mwingi sana.
- C. Kufanya shughuli mbalimbali.
- D. Wanaoitumia kufuata maagizo ya chombo hiki.

**42.** **"....tutaziweka bayana..."** Maana ya kauli hii jinsi ilivyotumika katika kifungu ni
- A. tutaziweka wasiwasi.
- B. tutazitoa jinsi zilivyo.
- C. tutaziweka wazi.
- D. tutaziweka panapostahili.

**43.** Kulingana na kifungu ulichosoma, maelekezo ambayo kompyuta hufuata huitwa
- A. sheria
- B. programu
- C. uongozi
- D. sahili

**44.** Jukumu la binadamu katika shughuli za kompyuta ni
- A. kukusanya habari.
- B. kuelekeza Kompyuta.
- C. kuiamsha Kompyuta.
- D. kuhifadhi habari.

**45.** Mwandishi anaifananisha kompyuta na binadamu kwa kuwa
- A. wanadamu wanawasiliana.
- B. kuna mawasiliano baina ya kompyuta.
- C. kompyuta na mwanadamu huwasiliana.
- D. wanadamu hawawasiliani.

**46.** Taarifa zinazoonyesha maelezo au takwimu baada ya kushughulikiwa katika kompyuta huitwa
- A. zao
- B. taarifa
- C. data
- D. habari

**47.** Aina mbili za diski ni
- A. tepetevu na ngumu.
- B. tepetevu na ya muda.
- C. ya tarakilishi na ya kompyuta.
- D. ngumu na programu.

**48.** Uwezo wa kompyuta kuhifadhi maktaba nzima unadhihirisha
- A. ubunifu wa mwanadamu.
- B. maendeleo katika teknolojia.
- C. sifa tele za binadamu.
- D. bidii za kompyuta.

**49.** Kompyuta ndiyo
- A. tarakilishi
- B. rununu
- C. mwengoya
- D. kipepesi

**50.** Kulingana na shughuli inazotekeleza kompyuta, inaweza kulinganishwa na sehemu gani ya binadamu?
- A. Akili
- B. Kichwa
- C. Maini
- D. Ubongo